# Sera ya Usaidizi wa Kifedha

CoxHealth inataka kuwasaidia wagonjwa wasio na bima ya afya au wanaohitaji usaidizi kulipia bili zao za hospitali. CoxHealth ni shirika lisilotafuta faida la huduma za afya, tunajali wagonjwa na jamii tunapohudumia kupitia huduma bora za afya bora na matibabu bora.
Wafanyakazi wetu wanaweza kukusaidia kufanya yafuatayo:

- Kutuma ombi la kupata bima ya afya kupitia Marketplace
- Kutuma ombi la kupata msaada wa Medicaid au msaada kwa Walemavu
- Kubaini ikiwa unastahili kupata Usaidizi wa Kifedha kutoka Cox Health

## Usaidizi wa Kifedha kutoka CoxHealth

Mwanzo kabisa, hali zako za kifedha hazitaathiri uwezekano wa kupokea huduma. Wagonjwa wote wanachukuliwa kwa heshima na usawa.
Wagonjwa wanaotimiza masharti fulani ya mapato wanaweza kupata Usaidizi wa Kifedha wa CoxHealth, ikiwamo ada za hospitali zilizopunguzwa na mipango ya kulipa.

Kwa kuzingatia **Kiambatisho cha 1,** wagonjwa wanaofaa kupata Usaidizi wa Kifedha watatozwa kiwago sawa ambacho kwa kawaida hutozwa watu wengine walio na bima ya huduma sawa. Maelezo kuhusu kiasi ambacho hutozwa kawaida na jinsi ya kuihesabu yanapatikana katika **Kiambatisho cha 1**, unapozungumza na Mshauri wa Kifedha au kwa kupiga simu katika namba zilizo hapa chini.

Usaidizi wa Kifedha utaanza kutekelezwa miezi 6 baada ya tarehe ya kuidhinishwa. Kutozingatia vigezo vya kustahiki kupokea Ufadhili wa Kifedha kutafanywa kwa kutegemea hali ya mtu binafsi.

## Masharti ya Kimatibabu ya Kupata Usaidizi wa Kifedha

CoxHealth itatoa huduma ya matibabu ya dharua kwa wagonjwa wote wanaotafuta huduma kama hizo bila ubaguzi na bila kujali kama wanaweza kulipa au
kama wanaweza kupata Usaidizi wa Kifedha. Huduma hiyo ni kwa mujibu wa Sheria ya Matibabu ya Dharura na Kujifungua (EMTALA).

Usaidizi wa Kifedha unapatikana tu kwa huduma za dharura na zinazofaa kimatibabu. Hautumiki kwa huduma za hiari kama vile upasuaji wa kurembesha. Pia hautumiki kulipia huduma ambazo umelipiwa kiasi fulani na washirika wengine kama vile mashirika ya bima au mpango wa serikali.

## Mwongozo wa Mapato kwa ajili ya Usaidizi wa Kifedha

Kiasi cha Usaidizi wa Kifedha unaopata unategemea maelezo ya Tathmini ya Kiwango cha Umaskini kwa mujibu wa serikali ya Marekani kila mwaka. Jedwali la kiwango cha Mapato na Mapunguzo kwa ajili ya Usaidizi wa Kifedha lipo katika **Kiambatisho cha 2**. Mbali na mapato yako, punguzo pia litazingatia ukibwa wa familia yako.

Orodha ya watoa huduma ambao wamejumuishwa kwenye Sera hii ipo katika **Kiambatisho cha 3**. Huduma nyingine zinazotozwa tofauti na baadhi ya watoa huduma, kama vile matabibu wa kijisiamamia, hayapo katika Sera ya Usaidizi wa Kifedha wa CoxHealth. Kwa orodha kamili ya watoa huduma hao, tafadhali angalia **Kiambatisho cha 4**. Pia unaweza kupata orodha hizi kwa kutumia taarifa zilizo hapa chini.

## Kuomba Usaidizi wa Kifedha

Unaweza kuomba Usaidizi wa Kifedha wakati wowote – kabla, wakati wa kupokea na baada ya huduma, ilimradi hazijapita siku 240 tangu ulipopokea bili yako kwa mara ya kwanza. Tunatuma maelezo ya jinsi ya kuomba usaidizi pamoja na bili yako. Pia kuna fomu ya kutuma ombi katika **Kiambatisho cha 5**, unapoiomba katika vituo vya CoxHealth, vikiwemo, vyumba vya dharura na mapokezi, au kwa kupiga simu katika namba zilizo hapa chini na kuomba nakala. Fomu ya kutuma ombi linahitaji thibitisho la mapato kama vile hati ya kuthibitisha kwamba ulilipa kodi ya mapato au stakabadhi ya kuonesha kiwango cha mshahara. Mifano ya hati ambazo unaweza kutumia kuthibitisha mapato yapo katika fomu ya kutuma ombi.

Wagonjwa ambao wana bima au wanastahiki kusajiliwa katika Medicaid wanaweza kupata Usaidizi wa Kifedha moja kwa moja kwa ajili ya matibabu ya dharura na huduma nyingine muhimu ya kimatibabu hospitalini zinazosimamiwa na Medicaid. Wagonjwa pia wanaweza kupata Usaidizi wa Kifedha kulingana na hali ya kifedha au ya kiuchumi katika jamii. Ustahiki wa aina hii ya usaidizi haumaanishi kwamba mgonjwa atapata usaidizi wa moja kwa moja siku za usoni.

**Completed applications may be returned to the hospital in person, by mail, or fax at:**

**CoxHealth**
Kwa: Washauri wa Kifedha
1423 N. Jefferson Ave.
Springfield, MO 65802
Pepesi 417-269-0518

**CoxHealth Branson**
Kwa: Washauri wa Kifedha
S.L.P 650
Branson, MO 65615
Pepesi 417-335-7071

**CoxHealth Monett**
Kwa: Washauri wa Kifedha
801 N. Lincoln Ave.
Monett, MO 65708
Pepesi 417-354-1185

**Hospitali ya Kaunti ya Cox Barton**
Kwa: Mratibu wa Rasilimali
29 NW 1st Lane
Lamar, MO 64759
Pepesi: 417-681-5266

au barua pepe kwa:
FinancialAssistanceApplications@CoxHealth.com

## Je, itachukua muda gani?

Unafaa kupokea majibu ndani ya siku 10 – 15 za kazi baada ya kukamilika kwa ombi lako. Ili kuhakikisha kwamba ombi lako linashughulikiwa ndani ya muda inavyostahili, ni muhimu sana uwasilishe hati zote zinazotakikana. Angalia fomu yetu ya kutuma ombi kwa maelezo zaidi.

## Nifanye nini kuhusu bili yangu wakati ninasubiri jibu?

Unafaa kuanzisha mpango wa kulipa kwa ushauriano na CoxHealth wakati ombi lako lingali linashughulikiwa.

## Makato

Ikiwa unawajibikia kulipa deni linalobaki baada ya Usaidizi wa Kifedha, CoxHealth itashirikiana nawe ili kupata mpangilio wa kulipa. Ikiwa si wewe utakayelipa malipo hayo na ukose kuwasiliana nasi, tunaweza kuhusisha shirika la kudai madeni ili kupata malipo hayo. Fahamu kile hatua hiyo inaweza kukusababishia kwa kusoma Sera ya Makato ya CoxHealth kwa kusoma **Kiambatisho cha 6**.

## Pata Maelezo Zaidi

Kwa maelezo zaidi kuhusu Usaidizi wa Kifedha wa CoxHealth, kutuma ombi au kuomba kupokea ilani kwa maandishi au kupitia barua pepe, unaweza kutembelea mojawapo ya idara zilizo katika maeneo yafuatayo ama unaweza kupiga simu ili uzungumze na Mshauri wetu wa Kifedha. Washauri wa Kifedha wa CoxHealth wapo ili kukusaidia kukamilisha kutuma ombi au kujibu maswali yoyote uliyo nayo kuhusu Sera ya Usaidizi wa Kifedha wa Cox Health:

**Vituo vya Afya vya Cox (Cox Kusini na Cox Kaskazini):**
Idara za Dharura au Mapokezi
3801 S. National Ave.
Springfield, MO 65807
417-269-0523

**Hospitali ya Tiba Mifupa na Viungo ya Meyer**
Idara ya Mapokezi
3535 S. National Ave.
Springfield, MO 65807
417-269-9800

**Kituo cha Afya cha Cox Branson:**
Idara za Dharura au Mapokezi
525 Branson Landing Blvd,
Branson, MO 65616
417-348-8930

**Hospitali ya Cox Monett:**
Idara za Dharura au Mapokezi
801 N Lincoln Ave.
Monett, Mo 65708
417-354-1118

**Hospitali ya Kaunti ya Cox Barton**
Idara za Dharura au Mapokezi
29 NW 1st Lane
Lamar, MO 64759
417-681-5100

Additional information and application forms are available online at **www.coxhealth.com.**

## Arifa

Katika juhudu za kufanya wagonjwa wetu, familia na jamii kufahamu Sera ya Usaizidi wa Kifedha wa CoxHealth, tumechukua hatua ya kuhakikisha sera hii inawafikia watu wengi iwezekanavyo kwa kubandika mabango katika maeneo ya mapokezi na usajili, ikiwa ni pamoja na katika Idara za Dharua, na kwa kusambaza maelezo kwa barua, katika kliniki za matabibu na maeneo mengine ya umaa. Vilevile Sera ya Usaidizi wa Kifedha, iliyoandikwa kwa lugha ya moja kwa moja, na fomu ya kuomba Usaidizi wa Kifedha, zinapatikana kwa lugha za Kiingereza, Kihispania, Kiburma, Kiswahili, Kivietnamu, Kialbania, Kirusi, Kiromania, Kireno, Kipolandi, Kikaren, Kichina, Kihmong, Kimarshall na Kimandarini.

**Kuanzia 11/2018**